Swahili

# Karatasi ya Ukweli 2

# Mpango wa Bima ya Taifa ya Ulemavu?

**Karatasi hii imeandaliwa na Amparo Advocacy ili kuwapa watu wa kutoka tamaduni na jamii za kilugha tofauti na taarifa zilizotafsiriwa kuhusu Mpango wa Bima ya Taifa ya Ulemavu.**

**Mpango wa Bima ya Taifa ya Ulemavu** unaitwa NDIS na ni njia mpya ya kuwasaidia watu wenye ulemavu kuwapata huduma na msaada wanaouhitaji. Ni bure, mfumo wa kitaifa hivyo itakuwa sawa kwa watu wote nchini Australia. Itakuwa inapatikana nchini kote katika 2019, na kuanza katika Queensland mwaka 2016. Watu wenye ulemavu ambao wanapata msaada kutoka NDIS wanaitwa 'washiriki'.

## Ustahili

**NDIS ni kwa ajili ya watu wenye ulemavu ambao wanaishi katika Australia na-**

- Wako chini ya umri wa miaka 65 wakati wanapata kwa mara ya kwanza NDIS
- Ni raia wa Australia **AU** wakazi wa kudumu, **AU** raia wa New Zealand ambao wanalindwa na visa Maalum ya wamiliki
- Wana ulemavu ambao hautaisha, ni 'wa maisha' na huathiri uwezo wao wa kushiriki katika shughuli za kila siku.

Kwa watu ambao hawastahiki, NDIS inaweza kuwa na uwezo wa kuwaunganisha na kupata misaada mingine inayofaa.

## Uchaguzi na Kudhibiti



Katika siku za nyuma, watu wengi wenye ulemavu katika Australia mara nyingi walionekana kutengwa katika maisha ya jamii, na walikuwa na uchaguzi mdogo jinsi misaada yao ilivyokuwa inatolewa. Katika NDIS, washiriki wanaweza kuamua ni misaada gani wanataka na namna ya kuipokea.

## Msaada wa busara na muhimu

NDIS italipia msaada unaohusiana na ulemavu, ambao ni lazima, na itasaidia mtu kufikia malengo na ndoto zao, na kuwasaidia watu kuwa huru zaidi.



**NDIS hutoa misaada ya watu wanaohitaji kuwa sehemu ya maisha ya kijamii na kiuchumi ya jumuiya yao.** Hii inaweza kuwa ni pamoja na-

- Kufanya mahusiano na hisia kushikamana na wengine - kuwa na familia na marafiki
- Kujiunga katika jamii na shughuli za kijamii - ikiwa ni pamoja na shughuli za burudani
- Kwenda shule, kusoma na kuwa na mafunzo - kama vile kusoma katika TAFE au Chuo Kikuu
- Shughuli za maisha ya kila siku - kama vile kufanya maamuzi, kulipa bili, na kutatua tatizo
- Mawasiliano - kama vile kuwasiliana na kuelewana na wengine
- Kutembea - kama vile kutembea kuzunguka nyumba yako na jamii, au kupata vifaa au visaidizi vya kufanya hivyo
- Mahitaji binafsi ya huduma na afya ya pekee - kama vile msaada wa kuoga, kuvalishwana kula chakula
- Shughuli za nyumbani - kama vile kuandaa chakula na kusafisha nyumba yako
- Ajira - kama vile kutafuta au kutunza kazi

## Kitu ambacho NDIS haitafadhili

NDIS haitafadhili kitu chochote ambacho-

- hakihusiani na ulemavu wa mtu
- kinahusiana na gharama za kila siku za kuishi ambazo hazihusiani na msaada binafsi wa mtu
- zinapaswa kulipiwa na shirika jingine, kama vile elimu, afya au nyumba
- zina uwezekano wa kusababisha madhara kwa mshiriki au kwa wengine.

## Watoto wenye ulemavu



NDIS inaweza pia kukusaidia kupata msaada wa mapema kwa mtoto mwenye ulemavu. Msaada wa mapema unaweza kusaidia kupunguza madhara ya muda mrefu ya ulemavu juu ya wewe au mtoto wako. NDIS inaita hii 'kuingilia mapema'.

## Watu wenye ulemavu na familia zao

Mahitaji ya watu wenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na uchaguzi na maamuzi yao ni muhimu katika NDIS kufanya mpango wa kuwasaidia, lakini jukumu la familia ni muhimu pia.

Watu wenye ulemavu wanaweza kukaribisha familia na wafuasi wengine ili kuwasaidia mchakato wa mipango ya NDIS. Mpangaji atafikiria kuhusu njia za kusaidia familia kutoa msaada unaoendelea na kuzingatia jukumu la familia wakati wa kufanya mipango na washiriki, ikiwa ni pamoja na msaada utakaotolewa, majukumu mengine, na mipango maisha yao yenyewe. Wapangaji wa NDIS pia huzingatia kwamba watu wenye ulemavu hutaka msaada wa familia kwa kutoa maamuzi sahihi, na wao kuthamini maoni yao, ujuzi na uzoefu.

## Kama unahitaji mkalimani

Ikiwa unahitaji mkalimani kuuliza swali au kujua zaidi, piga simu kwa TIS 131 450 na kuuliza kwa kuwa na uhusiano na Mpango wa Bima ya Taifa ya Ulemavu, 1800 800 110.

Interpreter

## Jinsi ya kujua kama unastahiki

Unaweza kutumia NDIS Kupata orodha kuona kama unaweza kuwa na haki ya kupokea misaada kutoka NDIS. http://www.ndis.gov.au/ndis-access-checklist

Wakati NDIS itakapoanza katika Queensland, watu wenye ulemavu wataweza kukamilisha 'Fomu ya Ombi la Kusaidiwa'. Fomu itatoa taarifa za NDIS za kuamua kama unaweza kupata msaada kutoka kwa NDIS. Kwenye fomu unahitaji kutoa taarifa kuhusu ulemavu wako, umri wako na uraia wako / ukaazi katika Australia. Nakala za fomu na aina ya taarifa na nyaraka unazohitaji kutoa kwa msaada wa ombi lako (kwa mfano ushahidi wa ulemavu, ukaazi, umri na kadhalika) zinapatikana kwenye tovuti ya NDIS (chini ya kifungu cha Mshiriki).

## Kabla ya kupanga

Watu wanaweza kuanza kufikiri na kupanga sasa kuhusu jinsi wanavyoweza kuishi maisha yao na msaada wanaouhitaji ili kufanya hivyo. Kuna kitabu cha mipango cha NDIS ambacho watu wanaweza kukamilisha kuwasaidia kuwa tayari kwa ajili ya mchakato wa mipango. Nakala za kitabu ziko kwenye tovuti ya NDIS. Hii imeweza kutafsiriwa katika lugha nyingi zifuatazo Hispania, Vietnam, Kiarabu, Kigiriki, Italia, na Kichina rahisi na jadi.

## Kufanya kazi na wapangaji wa NDIS

Wakati umearifiwa kwamba unastahili kwa NDIS utapata kijitabu cha mipango. Kijitabu cha mipango kinaelezea mipango na tathmini ya mchakato na ni pamoja na tamko la mshiriki kwamba lazima kukamilika kabla ya kupanga na tathmini ya mchakato. Kama watu wanahitaji msaada huo kama mkalimani au vifaa vilivyotafsiriwa, NDIS inaweza kusaidia kuandaa hii. Unaweza pia kuomba kuwa na vifaa vya kutafsiriwa kama unavihitaji kwa ajiri ya mikutano hii.

Kutakuwa na njia mbalimbali unaweza kuendeleza mpango wako wa NDIS, ikiwa ni pamoja na mkutano na mpangaji wa NDIS. NDIS inakusaidia kujadili mahitaji yako, malengo na matarajio na misaada unayoipokea. Hii inaweza kuchukua mazungumzo zaidi ya moja na unaweza kuleta mtu wa kukusaidia. Kutumia habari hii, NDIS itaandaa mpango wa misaada bora inayokutana na mahitaji yako na malengo yako. Unaweza kualika watu wengine ili kusaidia na kukusaidia wakati wa mchakato wa upangaji.

Kwa habari ziaidi www.ndis.gov.au

**Habari hii imekuwa imeandaliwa na Amparo Advocacy Inc.**

*Wakati kila hatua imechukuliwa kuhakikisha kuwa ni sahihi wakati wa uchapishaji, nyenzo hii ina maana ya kutoa maelezo ya jumla lakini inaweza isiwe sahihi, sasa au kamili kwa hali yako. Ushauri wa mtu binafsi unapendekeza zaidi.*

Tarehe: Novemba 2015

Funded by Queensland Government

Community Resource Unit Inc. Expanding Ideas; Creating Change

mamre ASSOCIATION INC

QDN QUEENSLANDERS WITH DISABILITY NETWORK

AMPARO Advocacy inc

53 Prospect Road, Gaythorne, QLD 4051
PO Box 2065, Brookside Centre, QLD 4053
www.amparo.org.au info@amparo.org.au

phone 07 3354 4900
Interpreter Service 131450